



HUMAN
RIGHTS
WATCH

NDOA ZA UTOTONI: TANZANIA

PICHA NA MARCUS BLEASDALE/VII KWA AJILI YA HUMAN RIGHTS WATCH

Tigisi, sasa ana miaka 12, alilazimishwa kuolewa akiwa na miaka 9, lakini sasa anahudhuria shule ya bweni kwa msaada wa NAFGEM, shirika la mahalia. Simanjiro, Tanzania. Agosti 9, 2014.



SUMMARY

Matilda H. alipokuwa na miaka 14, baba yake alimwambia kuwa anataka Matilda aolewe na mwanaume wa miaka 34 ambaye tayari alikuwa na mke mmoja. Baba yake Matilda alimwambia kwamba amekwisha poka mahari ya ng’ombe 4 na Shilingi za Kitanzania 700,000 (Tsh) (Dola za kimarekani 435).

Ingawa Matilda alifaulu mitihani yake na alikubaliwa kujiunga shule ya sekondari, baba yake alimwambia: “Hauwezi kuendelea na elimu yako. Inabidi uolewe kwa sababu huyu mwanaume amekwisha kukulilipia mahari.” Matilda alimbembeleza baba yake amruhusu aendelee na elimu yake, lakini alikataa.

Matilda alituambia, “Nina huzuni sana. Sikuweza kwenda shule, mahari ililipwa, na sikuweza kutokumtii baba yangu. Sikumfahamu mume wangu kabla.” Matilda alisema mama yake alijaribu kutafuta msaada kutoka kwa viongozi wa kijiji ili kuzuia ndoa, lakini “viongozi wa kijiji waliunga mkono uamuzi wa baba yangu kunioza mimi. Sikuwa na cha kufanya. Sikuwa na jinsi ila kukubali kuolewa.”

Mume wa Matilda alimfanyia ukatili wa kimwili na kingono na hakuweza kumtunza. Alituambia, “Mume wangu alikuwa masikini sana. Nilipoumwa, hakuwa hata na pesa ya kunipeleka hospitali.”

Katika Tanzania, wasichana 4 kati ya 10 wanaolewa kabla ya kutimiza miaka 18. Utafiti iliyofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) ulikadiria kuwa asilimia 37 ya wanawake wa Kitanzania wenye umri wa miaka kati ya 20-24 waliolewa kwa mara ya kwanza au walikuwa kwenye mahusiano kabla ya kutimiza



miaka 18, kati ya 2000-2011. Human Rights Watch imenukuu kesi ambapo wasichana wenye umri wa hata miaka saba walioolewa.

Ndoa ya utotoni imesimikwa kwenye jamii ya Tanzania. Kwenye tamaduni nyingi za Kitanzania, wasichana wanadhaniwa kuwa tayari kuolewa wanapobalehe na ndoa inaonekana kama njia ya kuwalinda dhidi ya ngono na mimba za kabla ya ndoa ambazo zinashusha heshima ya familia na kuweza kushusha kiasi cha mahari ambayo familia itapokea. Utendaji wa kitamaduni kama ukeketaji wa wanawake pia unapelekea kuwepo ndoa za utotoni kwenye baadhi ya jamii. Baina ya makabila ya Wamasai na Wagogo, ambapo Human Rights Watch ilifanya baadhi ya utafiti kwa ajili ya ripoti hii, ukeketaji unahusika kwa ukaribu na ndoa za utotoni na unafanywa kama sehemu ya jando la kuwaandaa wasichana, wenye miaka 10-15, kwa ajili ya ndoa.

Watanzania wengi wanaona ndoa za utotoni kama namna ya kupata usalama wa kifedha kwao na kwa mabinti zao. Mila ya mwanaume kulipa mahari kwa familia ya mke ni motisha muhimu kwa familia nyingi kuwaozesha mabinti zao. Baadhi ya wasichana wanaona ndoa kama njia ya kutoka kwenye umasikini, ukatili, au utelekezaji. Utumikishwaji wa watoto Tanzania inaweza kuhusika pia na kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha kuolewa kwa umri mdogo zaidi, kwa vile wasichana wanaokabiliana na unyanyasaji na utumikishwaji kwenye mahali pao pa kazi wanaona ndoa kama njia ya kutoka kwenye mateso yao.

Human Rights Watch iliwafanyia mahojiano ya kina wasichana na wanawake kwenye wilaya 10 kwenye mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kilimanjaro, Arusha,

Dodoma, na Lindi ya Tanzania bara, pamoja na watumishi wa serikali, maafisa wa ustawi wa jamii, maafisa polisi wanaofanya kazi katika Madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto, walimu, maafisa watendaji wa kata na kijiji, wafanyakazi wa afya, na wataalam. Human Rights Watch ilipeleleza sababu zinazochangia ndoa za utotoni, madhara makubwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaohusiana na ndoa za utotoni, na hatari zinazowakabili wasichana wanaokataa kuolewa. Pia tuliangalia mapengo kwenye mfumo wa hifadhi ya mtoto, ukosekanaji wa hifadhi kwa wahanga wa ndoa za utotoni, na vipingamizi vingi vinavyowakabili wakijaribu kupata haki, pamoja na mapungufu kwenye sheria zilizopo na mipango ya kupambana na ndoa za utotoni.

Kwa kuruhusu ndoa za utotoni, serikali inawajibika kwa madhara makubwa yanayowapata wasichana na wanawake, hivyo kukiuka haki nyingi za binadamu zinazotambulika chini ya sheria ya kimataifa. Wasichana wanaoolewa wakiwa watoto mara nyingi huwa wanashindwa kuendelea na masomo na matokeo yake wanatarajia kupata ajira yenye kipato cha chini kwa sababu ya kukosa elimu. Wasichana wanaweza kufanyiwa ukatili wa nyumbani na kubakwa ndani ya ndoa, na kupata msaada mdogo au kukosa msaada kabisa wakiwa kwenye ndoa yao au wanapoondoka. Wanalazimishwa kuingia kwenye utu uzima kabla hawajakomaa kimwili na kihisia na wanahangaika na athari za kimwili na za kihisia za kupata mimba wakiwa na umri mdogo. Athari hizi mbaya zinawadhuru zaidi wasichana wanaoolewa wakiwa na umri mdogo zaidi.

Ripoti hii inanukuu athari kubwa ya ndoa za utotoni kwenye elimu ya wasichana. Ndoa za utotoni zinadhoofisha upatikanaji wa elimu-

zinazuia fursa za kimaisha za wasichana na uwezo wao wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu maisha yao. Wasichana waliambia Human Rights Watch kwamba wazazi au walezi wao waliwatoa shuleni ili waolewe, na waliona vigumu kurudi shule baada ya kuolewa. Wasichana waliopata mimba au walioolewa mara nyingi walifukuzwa shule. Sera ya serikali ya Tanzania inaruhusu shule kuwafukuza au kukatisha masomo ya wanafunzi walioolewa au waliofanya kosa lililo “kinyume na maadili mema,” ambalo mara nyingi hujulikana kumaanisha kufanya ngono au kupata mimba kabla ya ndoa. Shule za Kitanzania hufanya vipimo vya lazima vya mimba kwa wasichana mara kwa mara, ambao ni ukiukwaji mkubwa wa haki yao ya faragha, usawa, na uhuru.

Wasichana ambao Human Rights Watch iliwahoji waliokataa au waliojaribu kukataa kuolewa walishambuliwa, walidhalilishwa kwa maneno, au walifukuzwa nyumbani na familia zao. Wengine walioshindwa kukwepa ndoa, wameeleza jinsi waume zao walivyowapiga na kuwabaka na hawakuwaruhusu kufanya uamuzi wowote nyumbani. Idadi kubwa wamesema pia kuwa waume zao waliwatelekeza na kuwaacha kuwatunza watoto bila msaada wowote wa kifedha. Wengi wamesema kuwa pia walipitia ukatili na unyanyasaji mikononi mwa wakwe zao.

Pia wasichana wengi waliambia Human Rights Watch jinsi walivyojihisi wapweke na kutengwa, wakilazimika kubaki nyumbani na majukumu ya nyumbani na kulea watoto au kwa sababu waume na wake zao kuzuia mienendo yao. Kutengwa na kuisha kwa ghafla kwa utoto wao, kitu ambacho mara nyingi kinahusika na ndoa za utotoni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, wa maneno na kingono

ambao wasichana walioolewa wanapitia, kukosa msaada pale wasichana wanapotafuta msaada kutoka kwa vyombo vya dola na familia, pamoja na shinikizo la kiuchumi na kitamaduni ambalo linazuia baadhi ya wasichana kuondoka kutoka kwenye ndoa zenye unyanyasaji, zina athari kubwa kwa afya ya kisaikolojia ya msichana. Wasichana wengi waliohojiwa na Human Rights Watch wamesema hawakuwa na furaha kwenye ndoa zao na wanajuta kuolewa mapema. Baadhi yao wamesema wamefikiria kuhusu kujiua.

Wafanyakazi wa afya wameelezea matokeo mabaya ya uzazi kwa wasichana na watoto wao pale wasichana wanapojifungua, pamoja na vifo vya wajawazito, fistula, kujifungua kabla ya muda, utapiamlo, na kupungukiwa damu. Huduma za afya za kabla na baada ya kujifungua, hususan kwenye maeneo ya Tanzania vijijini, ni haba, hivyo kuongeza hatari.

Kwa heshima yake, serikali ya Tanzania imefanya maboresho muhimu ya kisheria na sera kwenye eneo la haki za binadamu za wasichana na wanawake. Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana iliyopitishwa mwaka 1998, inaweka kubaka, utumikishwaji kingono wa watoto na ukeketaji wa wanawake kuwa makosa ya jinai na imeweka umri wa kuridhia tendo la ngono kuwa miaka 18. Pia, mnamo mwezi Juni mwaka 2014 bunge lilipitisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inayoruhusu wasichana kurudi shule baada ya kujifungua. Sera hiyo haishughulikii wasichana walioolewa, ingawa inataja kwamba wasichana wanaokatisha masomo kwa “sababu nyingine” pia waruhusiwe kurudi shule. Serikali imeandaa mipango kazi ya kitaifa ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Mnamo Oktoba 2014, Bunge Maalum la

Katiba la Tanzania limepitisha rasimu ya mwisho ya katiba mpya inayopendekezwa ambayo inajumuisha kipengele kinachotoa fasili ya mtoto kuwa kila mtu aliye chini ya umri wa miaka 18. Hata hivyo rasimu hiyo ya mwisho imeshindwa kuweka miaka 18 kuwa umri mdogo kwa wavulana na wasichana kuo au kuolewa.

Hata hivyo, sheria za Tanzania zinaruhusu ndoa za watoto kwa wasichana na hazitoi ulinzi wa kutosha dhidi ya ukatili wa nyumbani. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaweka miaka 18 kuwa umri mdogo ambao wavulana wanaruhusiwa kuo, lakini imeweka umri wa miaka 15 kwa wasichana kuolewa kwa ridhaa ya wazazi. Sheria zilizopo zinapingana na wakati mwigine haziko wazi, zikishindwa kufafanua mtoto ni nani kwa madhubuti. Serikali bado haijafanya mapitio ya Sheria ya Ndoa ili kutoa ulinzi dhidi ya ndoa za utotoni, ingawa iliashiria kwamba itafanya hivyo. Pia, mipango kazi ya serikali ya kushughulikia ukatili dhidi ya wanawake na watoto haiweki mikakati ya kina kukabiliana na ndoa za utotoni.

Tanzania ina kiwango kidogo sana cha uwajibikaji kwa wahanga wa ukatili unaohusiana na ndoa za utotoni, ikiwemo ukatili wa nyumbani. Tanzania haina sheria ya kina juu ya ukatili wa nyumbani na ubakaji kwenye ndoa sio kinyume cha sheria. Serikali imefanya juhudi ndogo sana kwenye kupeleleza na kuwashtaki wakosaji. Sababu kuu kadhaa zimeimarisha hali hii ya kutokujali. Wasichana na wanawake wengi hawajui haki zao au hawajui watafute wapi msaada, isipokuwa kwenye familia zao au taasisi za kitamaduni. Wahanga wengine hawatoi taarifa ya ndoa ya kulazimishwa na kunyanyaswa kwenye ndoa kwa sababu hawana imani na mfumo wa sheria

na wanaogopa kulipiziwa kisasi kama wakiripoti familia zao au waume wao. Ukosefu wa sheria iliyo wazi kuhusu familia ina maana kwamba mambo mengi yanayohusu ndoa, talaka, malipo ya matunzo, na ukatili wa nyumbani yanashughulikiwa kupitia taratibu za kimila, ambazo zinabagua na mara nyingi hushindwa kutoa haki kwa wahanga.

Matatizo haya yanazidishwa na kudumishwa na kukosa uwezo na kutokupatikana kwa mfumo wa mahakama, msaada mdogo wa kisheria na ambao haujumuishi wahanga wa ukatili wa kijinsia, na mwitiko wa polisi wa kizembe na wenye kupuuza taarifa za ukatili dhidi ya wanawake. Zaidi ya hayo, ukosekanaji wa nyenzo na watumishi waliopata mafunzo, rushwa kwenye mfumo wa sheria, na tabia iliyoenea na iliyozoeleka ya kuwabagua wanawake zinadhoofisha uwajibikaji wa ukatili wa kijinsia. Pia Tanzania haina nyumba za salama za kutosha ambapo wahanga wa ndoa za utotoni na wahanga wa unyanyasaji mwingine unaohusu ndoa za utotoni wanaweza kupata hifadhi na usalama.

Serikali ya Tanzania haijafanya jitihada za kutosha kuwalinda watoto walio hatarini kuingia kwenye ndoa za utotoni na za kulazimishwa na kuwasaidia wahanga na msaada wa kisaikolojia, kijamii au kiuchumi ambao wanauhitaji sana. Mara nyingi wahanga wanahangaika na matokeo ya unyanyasaji waliotendewa, wakiwa peke yao. Zaidi ya hapo, wanapata msaada mdogo ili kufidia elimu yao waliyoipoteza au kuwasaidia kuandaa fursa za kujitunza wao wenyewe na watoto wao. Wakati baadhi ya vikundi vidogo na mashirika ya msaada ya kimataifa wanaendesha mipango, jitihada zao hazitoshi kufidia kushindwa kwa asasi

za kiserikali kupitisha mikakati ya kitaifa ya kushughulikia mahitaji mbalimbali ya wahanga.

Matokeo ya kushindwa huku na mapungufu haya ni wanawake wengi na watoto kuendelea kuhangaika na athari zenye uharibifu wa muda mrefu za ndoa za utotoni. Ndoa za utotoni zinadhuru wanawake na watoto binafsi (mmoja mmoja), lakini pia zinadhuru familia na jamii. Kushindwa kupambana na tatizo kuna uwezo mkubwa wa kuwa na athari mbaya kwa ubaadae wa maendeleo ya Tanzania kijamii na kiuchumi.

Human Rights Watch inatoa wito kwa serikali ya Tanzania kuchukua hatua za papo kwa hapo na za kipindi kirefu kuwahifadhi wasichana na wanawake dhidi ya ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa na kuhakikisha haki zao za kibinadamu zinatimizwa, sambamba na wajibu wake wa kimataifa wa kuhifadhi haki za binadamu. Uchambuzi wowote wa hivi karibuni wa mikakati ya kitaifa juu ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto unatoa fursa kwa serikali kuimarisha hifadhi dhidi ya ndoa za utotoni na za kulazimishwa.

Pion H., 12, alikuwa na umri wa miaka 10 baba yake alipojaribu kumlazimisha akeketwe na aolewe na mwanaume aliyemzidi sana umri. Pion H. alikataa ndoa na alisema anataka kuendelea na elimu. Akiwa anashinikizwa na familia yake aolewe, Pion H. alienda kwa mwalimu wake wa shule kwa msaada. Mwalimu aliwasiliana na shirika la mahalia, NAFGEM, ambalo liliingilia kati kwenye familia yake na kuzuia asikeketwe na kuolewa. Sasa anasoma shule. Moshi, Tanzania. Agosti 7, 2014.



Anita, 19, alilazimishwa na baba yake kuacha shule na kuelewa alipokuwa na umri wa miaka 16. Anita na mama yake walipopinga ndoa hiyo, baba yake alikasirika na kuwapiga wote wawili, akisema kwamba amekwisha pokea mahari kwa ajili ya ndoa. Moshi, Tanzania. Agosti 7, 2014.



MAHARI

Mahari ni sababu kubwa inayopelekea ndoa za utotoni ndani ya Tanzania. Mahari inaamuliwa kati ya mwanaume na familia yake na inalipwa kwa familia ya mwanamke kwa namna ya pesa, ng’ombe au mifugo mingine, au mchanganyiko wa vyote viwili. Ingawa ni kitu cha kawaida kwenye jamii nyingi ndani ya Tanzania, mahari zinatofautiana kati ya kabila, uwezo wa familia, na sababu nyingine za kitamaduni na kijamii, kama weupe wa ngozi ya msichana au kama amekeketwa.

Mahari inaaminika na baadhi ya jamii kumpa mume na familia yake “haki ya umiliki” juu ya mke. Mahari inaweza kuongeza uwezekano wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao wanashindwa kutoka kwenye mahusiano yenye ukatili kwa sababu hawawezi kumudu kulipa mahari. Dora P. aliiambia Human Rights Watch kwamba mume wake alimfanyia ukatili wa kimwili na wa maneno, na kwamba muda wowote alipolalamika, alimjibu, “Nimekununua. Baba yako amechukua mali yangu kwa hiyo ninakumiliki. Unadhani unaweza kwenda popote?”

Mvulana anachunga ng'ombe. Ng'ombe au mifugo mingine mara nyingi huwa ni sehemu ya mahari. Moshi, Tanzania. Agosti 6, 2014.



UKEKETEJI WA WANAWAKE

Ndani ya Tanzania, ukeketaji wa wanawake unafanyika kwa sababu mbalimbali za kijamii na kitamaduni kutegemeana na kabila, kujumuisha kama sehemu ya jando la kumuandaa kuwa mwanamke. Baina ya makabila ya Wamaasai na Wagogo, ambapo Human Rights Wach ilifanya utafiti wake, ukeketaji wa wanawake unahusika kwa ukaribu na ndoa za utotoni na unafanyika kimsingi kama jando la kuwaandaa wasichana kwa ajili ya ndoa.

Kiongozi wa kimila wa Kimaasai, Laizer Daudi, aliiambia Human Rights Watch, “Kwenye jamii yetu, ni lazima kumtahiri msichana kabla hajaolewa. Wasichana wanatahiriwa kati ya miaka 10- 15 na wanaolewa miezi 2- 3 baada ya kutahiriwa, Kuna maumivu mengi unapochanganya ukeketaji, na ndoa ya kulazimisha kwa msichana.”

Pion H., 12, alikuwa na umri wa miaka 10 na anasoma darasa la pili shule ya msingi bibi yake alipomwambia atakeketwa na kuolewa:

Bibi yangu aliniambia, “Lazima uache shule sasa hivi. Jiandae kuwa mwanamke wa ‘kweli’ wa Kimaasai.” Nilianza kulia. Niliogopa. Nilijua (ukeketaji) utafanyika kwa sababu walimwambia dada yangu kitu hicho hicho. Naye pia alikuwa na miaka 10 walipomtahiri na kumlazimisha aolewe mwezi mmoja baadaye.

Msichana ambaye hajakeketwa anaweza kutengwa kijamii na kuitwa “takataka” au “hana faida.” Kama ameolewa, wakwe zake wanaweza kumlazimisha akeketwe. Baina ya makabila ya Kimaasai na Kigogo, msichana aliyekeketwa anatolewa mahari kubwa zaidi.

Clara, 17, alilazimishwa kukeketwa akiwa na miaka 9. Familia yake ilipomwambia atakeketwa, alijaribu kukimbia lakini alikamatwa na kurudishwa. Kilimanjaro, Tanzania. Agosti 8, 2014.





[kushoto] Wanawake wa Kimaasai wamesimama ndani ya kituo cha NAFGEM ndani ya Simanjiro. Sarah Elifuraha (kulia) alisema kuwa wasichana wanakeketwa ili kuandaliwa kwa ajili ya ndoa: “Kwenye jamii ya Wamaasai, msichana aliyekeketwa anaheshimika kwa sababu anatambulika kama amekua na amepitia jando. Niyo maana anakeketwa, ili aolewe.” Simanjiro, Tanzania. Agosti 9, 2014.

[chini] Rehema ana umri wa miaka 13 na anasoma shule ya msingi. Alisema kuwa wazazi wake walipanga kumkeketa, lakini alikataa kwa msaada wa shirika lisilo la kiserikali. Kilimanjaro, Tanzania. Agosti 8, 2014.





Barabara inayoelekea Simanjiro, ambapo jamii
nyingi za Kimaasai zinapatikana. Agosti 8, 2014.

UTUMIKISHWAJI WA WATOTO

Baina ya wasichana, utumukishwaji wa watoto unahusika na kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha uwezekano wa kuolewa katika umri mdogo zaidi. Tafiti ya mwaka 2008 ya Benki ya Dunia iliyoangalia matokeo ya utumukishwaji wa watoto kwenye vijiji vya Tanzania ilinukuu muunganiko kati ya utumukishwaji wa watoto na ndoa za utotoni, ikisema kuwa, “kadri watoto wanavyofanya kazi, kadri uwezekano wa wao kuelewa katika umri mdogo unavyozidi.” Wasichana wanaokabiliana na unyanyasaji katika mahali pao pa kazi wanaweza kuona ndoa kama njia ya kutoka kwenye mateso yao. Wasichana wanaofanya kazi wanapitia utumukishwaji wa kingono na unyanyasaji, na wakati mwingine wanaingia kwenye uhusiano na wavulana au wanaume ili kupata chakula au msaada mwignine, au kwa sababu wana mimba.

Human Rights Watch imewahoji wasichana 20 waliosema waliolewa wakiwa na umri mdogo ili kukimbia utumukishwaji wa watoto. Ndani ya Tanzania, kazi za nyumbani kwa watoto ni kitu cha kawaida na inakubalika kama njia ya kuchangia kwenye kipato cha familia. Pia inaweza kudhaniwa kuwa kama sehemu ya maadalizi ya msichana kwa ajili ya maisha ya baadaye ya ndoa. Kutokana na kanuni dhaifu za serikali juu ya ajira kwa watoto, wasichana wanakabiliana na unyanyasaji, ukiwemo unyanyasaji wa kimwili na kingono, na mara nyingi wanalipwa kidogo au hawalipwi kabisa.

Witness, mwenye miaka 19, alikuwa na miaka 14 na anasoma mwaka wa mwisho wa shule ya msingi baba yake alipomfukuza nyumbani kwa sababu alikuwa “amekua” vya kutosha kujitunza mwenyewe. Witness aliolewa muda mfupi baada ya kupata kazi ya baamed. Moshi, Tanzania. Agosti 6, 2014.



Watoto wanaangalia video kwenye shughuli ya jamii iliyofanywa na Mpango wa Agape wa Kudhibiti UKIMWI, shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi kutokomeza ndoa za utotoni. Shinyanga, Tanzania. Agosti 4, 2014.



MIMBA ZA UTOTONI

Tanzania ina asilimia kubwa za mimba ya wasichana wa shule. Kwa mujibu wa Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa Tanzania, “asilimia 44 ya wanawake huwa wamezaa au wana mimba ya mtoto wao wa kwanza wakiwa na miaka 19.”

Wasichana hawapati elimu ya kujamiiana na taarifa sahihi kuhusu dawa za kuzuia mimba. Pia wanaupatikanaji mdogo wa huduma ya afya ya uzazi na hawana nguvu ya kujadili ngono ya salama na wanaume ambao kwa kawaida huwa wanawavutia na pesa, zawadi na ahadi za kuwasomesha au kuwaoa.

Serikali ya Tanzania imeshindwa kuhakikisha upatikanaji wa elimu ya kina ya kujamiiana kwenye shule za msingi na sekondari, ingawa kuwepo kwa mpango wa “ujuzi wa kimaisha”- uliowekwa kwenye masomo yaliyopo, kama bayolojia, siasa, lugha, na ujuzi wa kazi- ambao unajumuisha taarifa kuhusu kujamiiana na uzazi wa mpango. Tanzania bara haina mtaala wa elimu ya taifa ya kujamiiana, ikimaanisha kuwa hakuna mwongozo ulio wazi kwa ajili ya shule au walimu kuhusu somo linahusu nini na vipi lifundishwe.

UKATILI WA NYUMBANI

Wasichana na wanawake wengi waliohojiwa na Human Rights Watch walisema kuwa wamafanyiwa ukatili kwenye ndoa zao.

Patricia J., 19, aliolewa na mwanaume wa miaka 18 alipokuwa na miaka 15, akitarajia kukimbia umaskini wa nyumbani. Mume wake alilipa mahari ya Shilingi za Kitanzania 7,000 (\$5). Hatimaye alitoka kwenye ndoa na sasa anaishi na rafiki:

Mume wangu alikuwa akinipiga karibia kila siku. Siku moja alirudi nyumbani na akaanza kupiga kelele na kutishia kuwa ataniunguza. Nilimuuliza kwa nini na akasema, “Baba yako amechukua pesa yangu kwa sababu ni maskini.” Aliniambia nipanue miguu yangu wazi. Nilikataa. Alitoka nje ya nyumba na akarudi ndani na mkaa unaowaka moto. Alipanua miguu yangu kwa nguvu na kusukuma mkaa wa moto ndani ya uke wangu. Sikuwa na cha kufanya. Nilichoweza kufanya ni kulia tu.

Mara nyingine wasichana hujaribu kuwaacha waume zao wakatili na kurudi kwenye familia zao, wakitarajia kupata msaada, lakini wasichana waliohojiwa na Human Rights Watch waliojaribu kurudia wenye familia zao walisema mara nyigni waliambiwa kuwa wanawake wote walioolewa wanapaswa kuvumilia unyanyasaji, na kisha wanalazimishwa kurudia kwa waume zao.

Rose aliolewa alipokuwa na miaka 16 na sasa ana watoto wawili. Mume wake alimpiga mara kwa mara na kumlazimisha afanye naye mapenzi. Rose amesema kuwa alifikiria kujiua ili kutoka kwenye ndoa hiyo. Moshi, Tanzania. Agosti 6, 2014.



Jacinta, 15, alikatishwa masomo baada ya viongozi kubaini kuwa ana mimba. Amesema walimu wake walimpeleka kwenye kituo cha afya kupima mimba. Alijifungua kabla ya muda wake na mtoto wake alifariki. Agosti 5, 2014.



KUZUIA WASICHANA WASIPATE ELIMU

Ndani ya Tanzania, mara nyingi ndoa hukatisha elimu ya wasichana. Wanafunzi walioolewa au wenye mimba wanafukuzwa shule au kukatishwa masomo mara kwa mara. Ingawa sio sera rasmi, shule za Kitanzania pia hupima mimba kwa lazima na kuwafukuza shule wasichana wenye mimba.

Human Rights Watch imewahoji wasichana kadhaa waliofukuzwa shule kwa sababu walikuwa na mimba. Wengine wamesema kuwa waliacha kuhudhuria shule baada ya kugundua wana mimba kwa kuhofia kufukuzwa shule.

Sharon J., 19, alifukuzwa shule alipokuwa mwaka wake wa mwisho wa shule ya msingi: “Mwalimu mkuu alipogundua kuwa nina mimba, aliniita ofisini kwake na kuniambia, “Unapaswa kuacha shule mara moja kwa sababu una mimba.” Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari ya Farkwa amesema, “Tunapombaini mwanafunzi mwenye mimba shuleni, tunaitisha kikao cha shule ambapo tunakubaliana kumfukuza shule mwanafunzi huyo.”

Utendaji wa kuwafukuza wasichana wenye mimba haujaruhusiwa moja kwa moja na sheria au sera, lakini serikali imefanya machache kuuzuia na ukiukwaji wa haki ya wasichana kupata elimu unaoambatana nao. Watumishi wa shule na serikali wanaweka utendaji wa kuwafukuza shule wasichana mwenye mimba kama sehemu ya jitihada za kuzuia mimba za utotoni, na kama hatua ya kinidhamu.



Angela, 15, amembeba mtoto wake mchanga wa kike kwenye hospitali ndani ya Tanzania. Hajaolewa na anaishi na wazazi wake, anatarajia kuendelea na masomo yake na siku moja awe nesi. Shinyanga, Tanzania. Agosti 4, 2014.



Sofia (katikati), 18, kwenye Kituo cha Mafunzo ya Ufundi cha Buhangija. Sofia alilazimishwa kuolewa na mama yake alipokuwa na miaka 14 na mwanaume ambaye alimpiga na kushindwa kumtunza kifedha yeye na watoto wake. Sasa Sofia anafanya kazi kumsaidia mama yake arudishe mahari. Shinyanga, Tanzania. Agosti 4, 2014.

MAPENDEKEZO

Kwa Rais wa Tanzania

- Alaani hadharani ukatili dhidi ya wanawake na watoto wanaokataa ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa.
- Aunge mkono hadharani kuwekwa kwa mfumo wa umri mdogo wa kuoa au kuolewa kwa wavulana na wasichana unaolingana na unaotambulika kimataifa kuwa miaka 18.
- Atoe wito kwa mamlaka za elimu kutokomeza utendaji wa kibaguzi wa kupima mimba kwa wasichana kwa lazima, kuwafukuza shule wasichana wenye mimba, na kukatisha masomo kwa wanafunzi walioolewa.

Kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

- Irekebishe Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili ijumuishe kifungu ambacho kinaruhusu wanafunzi walioolewa na wenye mimba kuendelea na elimu yao.
- Irekebishe muundo uliopo wa sheria na sera unaodhibiti kufukuzwa shuleni na kukatishwa masomo:
 - Irekebishe Kanuni Na. 4 ya Kanuni ya Elimu (Kufukuzwa Shule na Kukatishwa Masomo) ya 2002 kwa kuondoa “ndoa” kama sababu ya kufukuzwa shule, na kuongeza kifungu kinachosema wazi kwamba mimba na ndoa sio sababu ya mwanafunzi kufukuzwa shule au kukatishwa masomo.
 - Ihakikishe kuwa walimu na watumishi wa utawala wanafahamu kuwa kufukuzwa shuleni au kukatishwa masomo kwa sababu ya mimba na ndoa inakatazwa.
 - Ihakikishe kuwa wanafunzi wenye mimba na walioolewa wanaotaka kuendelea na elimu yao wanaruhusiwa na wanaweza kufanya hivyo katika mazingira yasiyo ya fedheha na ya kubaguliwa, na ifuatilie utii wa shule.

- Itokomeze upimaji wa mimba mashuleni na ihakikishe kuwa walimu na watumishi wa utawala wa shule wanaelewa kwamba utendaji huo umekatazwa.
- longeze upatikanaji wa elimu ya sekondari kwa kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu ya sekondari bila ya kujali matokeo ya Mitihani ya Kuhitimu Elimu ya Msingi. Hususan, iruhusu watoto waliofeli kurudia mtihani na kuomba kujiunga na shule za serikali.
- landae sekta ya elimu kwa ajili ya kuanzisha elimu ya lazima ya sekondari, kutokana na sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyopitishwa hivi karibuni. Hususan, shule zinapaswa kuwa na nyenzo za kuandikisha na kufundisha idadi kubwa zaidi ya wanafunzi.
- lanzishe mchakato wa kutambulisha mtaala wa elimu ya kujamiiana kwenye shule za msingi na sekondari unaofuata viwango vya haki ya binadamu. Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ifundishe mtaala huo kama somo linalofanyiwa mtihani, lililo huru, linalofundishwa na walimu waliopata mafunzo na wenye zana za kutosha, na kufuatilia utekelezaji wake.
- Iboreshe upatikanaji wa elimu kwa wasichana kwa:
 - Kuandaa mikakati ya kuwabakiza, kuhakikisha kuwa wasichana wanaoandikishwa shuleni wanabaki na wanamaliza shule, kama motisha kwa familia kuwabakiza wasichana shuleni, kutoa misaada ya masomo, kupanua mabweni ya kulala na mipango ya shule ya chakula, kuhakikisha shule zina usafi wa kutosha na kugharimia au kuondoa gharama za sare, vitabu, na gharama/ada nyingine. Ifanye hivi pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
 - Kupanua chaguo la matunzo ya mtoto na kukuza vituo vya kulea watoto

kwa ajili ya watoto wa wasichana walio na umri wa kwenda shule ili waweze kuhudhuria shuleni huku wakihakikisha kuwa watoto wao pia wanakua katika mazingira salama. Ifanye hivi pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, na Watoto na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

- Iboreshe ukusanyaji wa takwimu kwa idadi ya watoto wanaokatisha masomo kwa sababu ya kupata mimba na ndoa za utotoni ili kufanya vema tathmini ya athari ya sheria na sera mpya.
- Ibuni taratibu za kufuatilia kupitia shule, wasichana wanaositisha masomo, ili kupinga ndoa za utotoni, na kufuatilia wasichana waliositisha masomo kwa sababu ya mimba.
- Ipanue upatikanaji wa fursa za mafunzo ya ufundi kwa wanawake na wasichana walioolewa katika wilaya zote, na kutaarifu wananchi kuhusu kuwepo kwa mipango hii.
- Iweke adhabu kwa mamlaka za elimu zinazoshindwa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wakosaji wanaooa au kuwapa mimba wanafunzi.

Kwa Wizara ya Katiba na Sheria

- Ifanye kazi ili kuwa na uchambuzi wa kina na maboresho ya sheria ya Tanzania ya ndoa, kutengana, talaka, na mambo yanayohusika. Ifanye jitihada kupatanisha sheria ili kuweka uwazi na usawa kwenye utekelezaji kwa kutunga sheria ya kina ya familia na ndoa ambayo:
 - Inaweka kwa uwazi umri mdogo wa kuoa au kuolewa kwa wavulana na wasichana kuwa miaka 18.
 - Inatambua usawa wa ndoa zote, inahakikisha usawa wa haki ya kuolewa au kuoa, usawa kwenye ndoa, na wakati wa kuachana kwa wanandoa wote; na inatambua usawa wa haki hizi kwenye ndoa zote. Haki hizi

zinapaswa kujumuisha haki ya kumiliki na kurithi mali, na hifadhi ya watoto.

- Inaweka wazi vigezo vya ridhaa huru ya wenza wote kuoa au kuolewa, na inaondoa uhitaji wa ridhaa ya wazazi kwa ndoa kufungwa.
- Inaweka uthibitisho wa umri kuwa ni lazima kwa ndoa kufungwa.
- Inafanya uandikishaji wa ndoa kuwa ni lazima.
- Inaweka wazi adhabu kwa watu wazima wanaohusika kwenye kupanga, kufungisha na kuandikisha ndoa za utotoni au ndoa za kulazimishwa.
- Inakikisha kuwa wasichana walioolewa kabla ya kutungwa sheria mpya wana uamuzi wa kutoka kwenye ndoa hiyo, na inalinda haki zao mpya za kumiliki mali, kukaa na watoto, na kupata matunzo.
- Inaweka adhabu zilizo wazi kwa vitendo ya kikatili dhidi ya wanawake na watoto vinavyofanyika kama vitisho au malipizi ya kukataa kwao kuolewa; na inatoa huduma zinazotosheleza za sheria, afya, na kisaikolojia na kijamii kwa wahanga wa mashambulio haya.
- Inaweka kwamba wale walioolewa kwa kulazimishwa wakiwa watoto watakuwa na haki ya kufungua mashtaka ya kosa la jinai, kupata talaka, na kupata matunzo ya watoto.
- Inakataza ndoa za mke zaidi ya mmoja na inalinda haki na hadhi za wanawake waliokuwa kwenye ndoa za mke zaidi ya mmoja kabla ya kutungwa kwa sheria hii.
- Pale sheria mpya ya familia inapopitishwa, ifanye kampeni za kuelewesha wananchi kuhusu vifungu vya sheria, kwa kulenga kuongeza uelewa wa wananchi katika maeneo ya mjini na vijijini pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto.
- Ifanye jitihada katika kuzifuta sheria zote zinazobagua wanawake na watoto, pamoja

na zile zinazoruhusu matumizi ya sheria ya kimila kwenye mambo ya ndoa, talaka, na mirathi.

- Ichukue hatua muhimu ili kutunga sheria ya kina ya ukatili wa nyumbani. Sheria hiyo inapaswa kufanya ukatili wa nyumbani kuwa kinyume cha sheria.
- Iboreshe Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 itambue ukatili wa kingono ndani ya ndoa kama kosa la jinai, ikitaja hususan kwamba ndoa haitakuwa sababu ya kujitetea kwenye mashtaka ya shambulio la ngono.
- Upatikanaji zaidi wa huduma za msaada wa sheria kwenye maeneo ya mjini na vijijini, na ihakikishe kwamba huduma za msaada wa sheria ni pamoja na kusaidia kwenye kesi za ukatili dhidi ya wanawake, pamoja na ndoa za utotoni, za mapema na za kulazimishwa.
- Itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa polisi na waendesha mashtaka juu ya wajibu wao kupeleleza na kuendesha mashtaka ya ukatili dhidi ya wanawake, pamoja na ndoa ya utotoni na za kulazimishwa, chini ya sheria husika, kwa kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, na Wizara ya Katiba na Sheria.
- Ipeleleze shutuma za rushwa kuhusiana na kesi za ndoa za utotoni na, kama ushahidi utapatikana, iwaadhibu maafisa wa utekelezaji wa sheria wanaohusika.
- Ianzishe kanzi data (database) kuu ya ukatili dhidi ya wanawake ili kuweka kumbukumbu ya idadi na aina tofauti za kesi zinazotolewa taarifa pamoja na matokeo yao, kwa mfano rufaa kwenda taratibu za kimila, na ufuatiliaji kama amekutwa na hatia au ameachiwa huru. Ihakikishe takwimu hizo zinapatikana kwa wananchi.
- Ipanue mahakama za watoto, kama ilivyowekwa kwenye Sheria ya Mtoto, kwenye maeneo ya vijijini na mjini ili kuongeza upatikanaji wa haki kwa watoto.

- Iwajulishe wasichana na wanawake kuhusu haki zao za kupata matunzo ya watoto kutoka kwa baba wa watoto wao chini ya sheria husika, kwa kuratibu pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto.
- Ilimarishe muundo wa haki ya binadamu ndani ya Tanzania wa kuwahifadhi wanawake kwa ichukue hatua zinazopasa kuhakikisha kuridhiwa, bila kuchelewa wala kusita, kwa Mkataba Dhidi ya Mateso na Adhabu au Matendo Mengine ya Kikatili, yasiyo ya Kibinadamu au ya Kiudhalilishaji, na Mkataba wa Kuridhia Ndoa, Umri Mdogo wa Ndoa, na Uandikishaji wa Ndoa. Kutafuta msaada kwa ajili ya jambo hili kwenye wizara husika za serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto

- Ibuni mpango kazi wa taifa wa kupambana na ndoa za utotoni, kulingana na utendaji bora wa kimataifa, pamoja na mchango kutoka kwa vikundi vya haki ya wanawake na watoto, wataalam wa afya, na watoa huduma wengine; kuratibu jitihada kati ya wizara zote husika; itafute nyenzo za kutosha kuutekeleza mpango kazi huo.
- landae upya na kupanua Mpango Kazi wa Taifa wa Kuzuia na Kushughulikia Ukatili Dhidi ya Watoto ujumuishe mikakati ya kina kuzuia na kushughulikia ndoa za utotoni na za kulazimishwa, kulingana na utendaji bora wa kimataifa. Ihakikishe kuna mchango kutoka kwenye vikundi vya haki ya wanawake na watoto, wataalam wa afya, na watoa huduma wengine; iratibu jitihada kati ya wizara zote husika; itafute nyenzo za kutosha kuutekeleza mpango kazi huo.
- landae vituo vya misaada kwa simu, mabango, au nyenzo za mawasiliano

zinazofanana na hizo kuhakikisha kuna uelewa wa, na upatikanaji wa ushauri, hifadhi, na kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida watoto wote walio hatarini au waliopo ndani ya ndoa za kulazimishwa.

- Ihakikishe kuwa mipango inayoshughulikia mahitaji ya kisaikolojia na ya kijamii ya wanusurika wa ukatili wa kijinsia inajumuisha wahanga wa ndoa za utotoni na za kulazimishwa.
- Ipanue mipango kazi ya kuwawezesha wasichana na wanawake kuwa na shughuli zinazowaingizia kipato, hususan wasichana na wanawake waliotelekezwa na waume zao na familia zao, kwa kuratibu na wizara husika za serikali.
- landae na kutekeleza kampeni za kitaifa za kuelimisha jamii kuhusu ndoa za utotoni, za mapema na za kulazimishwa. Ifanye hivi kwa kushauriana na wizara husika za serikali, jamii, viongozi wa kimila na kidini, wanawake na wasichana, na asasi zisizo za kiserikali. Ijumuishe taarifa kuhusu:
 - Madhara ambayo ndoa za utotoni zinasababisha na faida za kusubiri kuolewa na kuzaa.
 - Majukumu ya watekelezaji wa sheria, hatua za hifadhi, tiba ya kisheria, na matunzo ya kiafya na kisaikolojia wanayopata wasichana na wanawake pamoja na haja ya wasichana kutoa taarifa ya ndoa za utotoni.
 - Matokeo kwa wakosaji.
 - Umuhimu wa elimu kwa wasichana.
 - Sababu nyingi zinazochangia mimba ya wasichana wa shule na fedheha inayozunguka mimba ya wasichana wa shule.
- Ianzishe nyumba nyingine zaidi za hifadhi, kama nyumba za salama, kwa wasichana na wanawake wanaotishiwa na ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa, au aina nyingine za ukatili wa kijinsia. Ihakikishe wasichana na wanawake wanaelewa kuhusu kuwepo kwa nyumba

za hifadhi, na jinsi ya kuzifikia.

- lunge mkono kuandaliwa kwa sera za elimu zinazozingatia masuala ya jinsia pamoja na, jitihada za kutambulisha elimu ya kina ya kujamiiana mashuleni, sera za kuzuia upimaji wa lazima wa mimba kwa wasichana wa shule na kufukuzwa kwao shule, pamoja na kukatishwa masomo kwa wasichana walioolewa.
- Ihakikishe kuwa maafisa wa ustawi wa jamii, kwa kushirikiana na wizara husika wanabaini na kuhifadhi watoto dhidi ya unyanyasaji wa watoto na utelekezaji, wanawachukua na kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida watoto waliotelekezwa, na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika. Ifanye hivi pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

- Ianzishe mchakato wa kutambulisha mtaala wa elimu ya kina ya kujamiiana kwenye shule za msingi na sekondari ambao unalingana na viwango vya kimataifa vya haki ya binadamu, pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.
- Ifundishe mtaala huo kama somo linalofanyiwa mtihani, lililo huru linalofundishwa na walimu waliopata mafunzo na wenye nyenzo za kutosha, na ifuatilie utekelezaji wake.
- Iboreshe upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na taarifa zake kwa wasichana na wanawake, pamoja na kupatikana kwa huduma za dharura za ukunga na mpango wa uzazi. Hususan, iongeze upatikanaji wa taarifa na ihakikishe huduma bora ya afya ya uzazi iliyo rafiki kwa vijana inatolewa kwenye wilaya zote.
- Iwapatie watoa huduma ya afya mafunzo stahiki kuhusu haki za uzazi na kujamiiana za vijana. Mafunzo yanapaswa kulenga

zaidi kwenye haki ya kupata taarifa na huduma, pamoja na uzazi wa mpango (dawa za kuzuia mimba), na uelewa wa sababu nyingi zinazolingiliana ambazo zinachangia watoto wa shule kupata mimba.

- Ihakikishe watoaji huduma za afya wanajulishwa kuwa kuwapima wasichana mimba kwa lazima ni kinyume na sheria, na kuhusu hoja ya kukiuka haki za binadamu.
- Ilimarishe uwezo wa watendaji wa jamii na serikali za mitaa kuhifadhi watoto walio katika mazingira magumu, wakiwemo watoto walio hatarini kufunga ndoa za utotoni na utumikishwaji wa watoto, na ihakikishe wanapata huduma za hifadhi ya mtoto.

Kwa Wizara ya Kazi na Ajira

- Ichukue hatua kutokomeza utumikishwaji wa watoto ambao unaodhoofisha upatikanaji wa elimu kwa watoto kama sehemu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Watoto. Hususan, iongeze ukaguzi wa utumikishwaji wa mtoto ikiwemo kwenye maeneo ya kazi yasiyo rasmi, na iendeshe mipango kazi ya kuwatoa watoto kutoka kwenye utumikishwaji wa watoto na kuwaandikisha shuleni au kwenye mafunzo ya ufundi. Pia, shughuli zinapaswa kujumuisha utoaji wa huduma stahiki za afya na, kama inabidi, hatua za kurudishwa kwenye jamii.
- Ifanye utafiti wa kitaifa kuhusu utumikishwaji wa watoto Tanzania, pamoja na Wizara ya Kazi na Ajira.

Kwa Wizara ya Mambo ya Ndani

- Ipanue madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto kwenye maeneo ya mijini na vijijini ndani ya Tanzania. Iongeze idadi ya maafisa katika madawati haya, ihakikishe mafunzo ya kutosha kuhusu ukatili wa

kijnsia yanatolewa kwa polisi wanaofanya kazi kwenye madawati haya, na itafute nyenzo za kutosha ili wafanye kazi zao.

- Itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa polisi na waendesha mashtaka juu wa wajibu wao kupeleleza na kuendesha mashtaka ya ukatili dhidi ya wanawake, ikiwemo ndoa za utotoni na za kulazimishwa, chini ya sheria husika, kwa kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Katiba na Sheria.
- Itoe adhabu stahiki au kuwafungulia mashtaka maafisa wa utekelezaji wa sheria wanaopokea rushwa.

Kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

- Izidishe ufuatiliaji wa kesi za ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa. Ipeleleze na kuchapisha ripoti juu ya hoja ya ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa, mapengo kwenye hifadhi ya wahanga, na upatikanaji wa haki kwa wahanga.

Kwa Umoja wa Afrika

- Isihi Tanzania ianzishe kampeni ya Umoja wa Afrika ya kutokomeza ndoa za utotoni, na kuandaa viashiria madhubuti kwa ajili ya kufuatilia na kupima maendeleo.

Kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Wafadhili wa Kimataifa

- Wasihi serikali ya Tanzania kutokomeza kukatisha masomo ya wanafunzi walioolewa au wenye mimba, na kutoa fursa za kujiunga tena shuleni kwa wasichana walioolewa na wasichana waliozaa wenye umri wa kwenda shule.
- Wasihi na kuunga mkono serikali ya Tanzania kuchukua hatua ili kuongeza upatikanaji wa elimu ya sekondari kwa kuchukua hatua zote zinazobidi ili kuhakikisha watoto wanaweza kupata elimu ya sekondari bila kujali matokeo

ya Mitihani ya Kuhitimu Elimu ya Msingi, na kuchukua hatua kuwaruhusu watoto wanaofeli kurudia mitihani na kujiunga na shule za serikali.

- Wasihi na kuunga mkono serikali ya Tanzania kuanzisha mtaala wa elimu ya kujamiiiana kwenye shule za msingi na sekondari ambao unafuata viwango vya kimataifa vya haki za binadamu; itekeleze mtaala huu kama somo lililo huru, linalofanyiwa mtihani.
- Waunge mkono maboresho ya sekta ya sheria ambayo yanalenga sana kwenye kushughulikia ubaguzi dhidi ya wanawake kwenye sheria na kwenye utendaji.
- Katika mipango kazi ambayo wanafadhili, wafadhili wanapaswa kutoa msaada kwenye kuweka mikakati ya kuzuia ndoa za utotoni, za mapema, na za kulazimishwa na kusaidia wasichana walioolewa. Mikakati hii inaweza kujumuisha mikakati ya kuboresha upatikanaji wa elimu kwa wasichana, pamoja na ile inayowawezesha wasichana walioolewa na wenye mimba kurudi shuleni, kuongeza upatikanaji wa taarifa na huduma za afya ya uzazi na kujamiiiana kwa wasichana waliobalehe, kufanya shughuli zinazowapatia kipato kwa wasichana na familia zao, ikiwa ni pamoja na wasichana walioolewa, kujenga uelewa kwa jamii kuhusu madhara ya ndoa za utotoni, na umuhimu wa kuolewa baadaye, na kuwasaidia wasichana walio hatarini kwa, na waliopo kwenye ndoa za kulazimishwa, kupata hifadhi, na haki.
- Wawezeshe kuanzishwa na kuendelezwa kwa Madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto Tanzania, wahakikishe kwamba yanapatikana kwenye maeneo ya mjini na vijijini nchini kote.
- Wawezeshe mashirika yasiyo ya kiserikali kutekeleza mipango kazi ili kuelewa vema sababu za msingi za ndoa za utotoni na za kulazimishwa Tanzania, na kufuatilia

na kufanya tathmini ya mipango kazi inayoshughulikia ndoa za utotoni na za kulazimishwa na kutumia taarifa hii kuboresha mipango kazi.

- Wawezeshe kuanzishwa na kuendelezwa kwa nyumba za salama kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia.
- Wasihi na wawezeshe serikali ya Tanzania kuanzisha na kutekeleza kampeni ya Umoja wa Afrika ya kutokomeza ndoa za utotoni, na kuandaa viashiria madhubuti kwa ajili ya ufuatiliaji na kupima maendeleo.
- Wawezeshe kupanuliwa kwa huduma za msaada wa kisheria kwenye maeneo ya mjini na vijijini, pamoja na kuipanua ijumuishe ukatili wa kijinsia.



Picha ya viongozi wa Kimaasai waliozimia kutokomeza ukeketaji wa wanawake na ndoa za utotoni kwenye jamii yao. Simanjiro, Tanzania. Agosti 11, 2014.

Majina bandia yalichaguliwa bila mpangilio rasmi, na yanaweza yasiwakilishe kabila na dini ya mhojiwa.

Aisha (si jina halisi) alikuwa na miaka 17 na alikuwa anasoma kidato cha tatu kwenye shule ya sekondari baba yake alipomlazimisha kuolewa na mwanaume wa miaka 45, ambaye alimpiga na kumbaka mara kwa mara. Shinyanga, Tanzania. Agosti 7, 2014.

© 2014 Marcus Bleasdale/VII kwa ajili ya Human Rights Watch